**HOTUBA YA WAZIRI WA NCHI (OFISI YA RAIS) TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA, MHE. SULEIMANI JAFFO WAKATI WA KUFUNGA KIKAO KAZI CHA MAAFISA HABARI, MAWASILIANO NA UHUSIANO SERIKALINI UKUMBI WA AICC, ARUSHA MACHI 16, 2017**

**Ndugu Susan Mlawi, Katibu Mkuu, Wizara ya Habari, Utamaduni, Sanaa na Michezo;**

**Ndugu Gabriel Daqqaro, Mkuu wa Wilaya ya Arusha ambaye pia ni Kaimu Mkuu wa Mkoa;**

**Dkt. Hassan Abbasi, Mkurugenzi, Idara ya Habari na Msemaji Mkuu wa Serikali;**

**Ndugu Paschal Shelutete, Mwenyekiti wa Chama cha Maafisa Habari Serikalini (TAGCO);**

**Watendaji mbalimbali waandamizi wa Serikali ambao wako nasi hapa;**

**Maafisa Habari Serikalini;**

**Waandishi wa Habari;**

**Mabibi na Mabwana;**

**Assalam aleikum.**

Awali ya yote napenda kuchukua fursa hii kumshukuru Mwenyezi Mungu mwingi wa rehema aliyetukutanisha hapa tukiwa na afya njema. Vilevile nitumie nafasi hii kuwashukuru kwa dhati waandaaji wa mkutano huu kwa kuona umuhimu wa kunikaribisha kufunga kikao hiki. Asanteni sana.

Aidha, ni imani yangu kuwa mmeishi salama kwa kipindi cha wiki moja mlipokuwa mnahudhuria kikao kazi hiki hapa Arusha na mmepata fursa ya kujadili nada mbalimbali katika kuboresha kazi zenu.

Napenda kutumia fursa hii kutoa shukrani zangu za dhati kwa uongozi wa Wizara ya Habari, Utamaduni, Sanaa na Michezo kwa kuratibu kikao hiki muhimu kwa taasisi zote za Serikali nchini kwa kushirikiana na Chama chenu cha Maafisa Mawasiliano Serikalini (TAGCO).

Nimetaarifiwa juu ya washiriki takribani 300 waliohudhuria katika kikao kazi hiki kutoka kila kona ya nchi yetu. Napenda mahsusi kabisa kuzipongeza ofisi zote za Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa ambazo ziliitikia wito kupitia barua iliyoandikwa na Katibu Mkuu-TAMISEMI wa kuwataka kuwalipia na kuwaruhusu maafisa wao wa habari kuhudhuria mafunzo haya. Wale ambao hawakutekeleza tutauliza na kufuatilia ni kwa nini maafisa wao hawakuhudhuria kikao kazi hiki muhimu?

***Ndugu washiriki,***

Hakika nakubaliana na Katibu Mkuu, Mama Susan Mlawi katika utangulizi wake kuwa kikao kazi cha mwaka huu kimekuwa na umuhimu wake katika kada ya mawasiliano nchini na hasa katika mawanda ya kuboresha mawasiliano ya kimkakati Serikalini.

Nimefurahi kusikia kwamba katika siku hizi tano (5) mlizokuwa hapa Arusha pamoja na shughuli za kijamii, miongoni mwa mada zilizowasilishwa ni kuhusu namna mnavyopaswa kuboresha utendaji wenu ili kuongeza weledi na kupanga mikakati ya namna bora ya kuimarisha mawasiliano Serikalini ikiwa ni pamoja na kuisemea Serikali katika nafasi zenu.

***Ndugu washiriki,***

Moja ya mambo ambayo TAMISEMI kwa sasa tunayafanyiakazi ni mageuzi makubwa katika utoaji wa huduma. Wizara yangu inadhamana ya kusimamia kwa karibu utoaji wa huduma nyingi n a za muhimu kwa wananchi kama vile maji, afya, elimu na nishati na hata utekelezaji wa Tanzania ya Viwanda.

Hivyo kwa upande wetu sisi katika hatua zote hizi za utoaji wa huduma tunaamini kwa dhati kuwa upo umuhimu wa wananchi kupata mrejesho wa nini kinafanywa na Serikali yao lakini na wao kupaza sauti zao pale ambapo panakwenda kombo.

Ni kwa sababu hii basi Afisa Habari hasa wale wa kwenye ofisi mbalimbali za Tamisemi ni muhimu sana kuwa wabunifu na watendaji wanaojituma katika kuonesha mafanikio ya utekeleza na kuyatetea lakini pia kuwa kiungo kati ya wananchi na Serikali yao.

Lazima uwezo ushirikiano wa karibu kati ya maafisa habari na watendaji wengine wa Serikali hasa viongozi katika Halmashauri na wataalamu mbalimbali.

**Changamoto Zilizopo**

Nimeelezwa katika maazimio yenu na mrejesho wa jumla nilioupata kuhusu kikao hiki kuwa moja ya changamoto inayokwaza kufikiwa ufanisi wa utoaji habari hasa katika mamlaka zilizoko chini ya Tamisemi ni pamoja na vifaa, kushirikishwa na zaidi kukosa ushirikiano kutoka kwa wataalamu na baadhi ya viongozi wa maeneo husika.

Kutokana na changamoto hizi, nachukua fursa hii kutoa maelekezo yafuatayo:

Mosi, Kuanzia mwaka ujao wa Bajeti  Makatibu Tawala na Wakurugenzi wa Halmashauri, Miji, Majiji na Manispaa waweke kipaumbele kwa kutenga fedha za kununua vifaa muhimu kwa ajili ya maafisa habari kama vile kompyuta na kamera;

Pili, Nawaagiza viongozi hao pia kuwapa ushirikiano wa kutosha maafisa habari ili waweze kuzitoa taarifa muhimu za Serikali kwa vyombo vya habari na wananchi kwa ujumla kwa wakati na bila vikwazo. Mahali popote ambapo Afisa Habari ataonekana kuwa hatimizi majukumu yake na ikabainika ni kwa sababu hapewi ushirikiano au anakwamishwa na watendaji wengine tutachukua hatua kali;

Nne, pamoja na hatua mbalimbali ambazo zimeshachukuliwa kufuatia maagizo ya ofisi yangu mwaka jana, bado kuna changamoto kwa baadhi ya maafisa habari kutoruhusiwa kuingia katika vikao muhimu vya uamuzi au kujadili maendeleo. Nawaangiza viongozi wote katika Tamisemi kutambua kuwa Afisa Habari ndiye mshauri mkuu katika eneo lao kuhusu masuala ya habari na anapaswa kuingia katika vikao vyote ili aelewe nini kinaendelea na kushauri; na

Nne, kazi yenu hii pia, kama alivyosema Waziri Dkt. Harrison Mwakyembe wakati wa ufunguzi, ni kazi ya kujituma sana, kuwa wabunifu na zaidi kujifunza kutoka kwa wengine. Nitumie fursa hii kusisitiza kuwa vile vile hatutawavumilia maafisa habari ambao wanapata mahitaji ya msingi lakini hawatimizi wajibu wao.

Sifa kubwa ya afisa habari ni kuwa na habari; ni kuijua taasisi yake kwa kina; ni kuhakikisha anaandaa tarifa na habari kitaalamu ili wananchi wajue nini kinaendelea na anatakiwa kuwa mbele kushauri viongozi wake kuhusu mikakati ya habari. Msipotimiza haya hamuitendei haki nchi yenu.

Serikali haitawavumilia maafisa habari wanaoshindwa kuendana na maendeleo ya teknolojia. Hapa nchini karibu nusu ya Watanzania wanatumia intaneti. Dunia pia takwimu zinaonesha kuwa asilimia 50 ya watu wanatumia mitandao ya kijamii.

Tunatarajia kuwa na maafisa habari wanaojua ukweli huu na kuitumia intaneti kufikisha tarifa kwa wananchi.

Tano, aidha, sote tunafahamu kuwa Serikali yetu ya Awamu ya Tano inatekeleza mambo mengi ya kimageuzi na yenye faida kwa wananchi na sisi TAMISEMI ndio kiini cha utekelezaji kwa sehemu kubwa. Nafahamu pia upo ugumu kwa Maafisa Habari ama kupata takwimu kutoka kwa wataalamu wetu au wakati mwingine wanapata nafasi ya kuwapeleka katika vipindi iwe vya redio au televisheni lakini wataalamu wetu pia wamakuwa wazito licha ya kuwa wao ndio wenye undani wa mambo mengi tunayotekeleza.

Nawaagiza wataalamu hao kutoa ushirikiano wanapopangiwa vipindi na maafisa habari na wawe wepesi kwenda kutoa mrejesho kwa wananchi kupitia vipindi hivyo maalum au hata kushirikiana na maafisa habari kuandaa mikutano na vyombo vya habari ya mara kwa mara katika maeneo yao.

Maagizo haya yatafikishwa kwa wahusika wote kwa maandishi na Ndugu Katibu Mkuu-Habari na Mkurugenzi wetu wa MAELEZO nitaomba mtukumbushe kila robo mwaka kujua utekelezaji wa maagizo haya unakwenda vipi. Kama mlivyoanza ninyi kupimana, nasi tutawapima watendaji wa TAMISEMI kwa namna wanavyotekeleza maagizo yanayohusu sekta ya habari na hususani maagizo ya kikao kazi hiki.

Ni matumaini yangu kuwa baada ya kikao kazi hiki na kwa maagizo na usimamizi tutakaoendelea kuuchukua katika kuboresha kazi zenu, mtaendelea kuongeza juhudi katika kuisemea serikali narejea tena, sisi tutawapigania muwe na mazingira bora zaidi ya kazi, lakini naji mkajiongeze.

***Ndugu washiriki,***

Nimeambiwa mwisho wa kikao chenu kuna maazimio kadha mmejiwekea; napenda kuwaasa, kama ambavyo tayari nimetoa maagizo hapo juu, Wizara yangu itakuwa tayari kutekeleza maazimio yote mliokubaliana yanayotuhusu TAMISEMI katika kikao kazi hiki ili kuweza kuimarisha utendaji kazi wenu.

Kabla sijafunga napenda niwapongeze Wizara ya Habari na TAGCO kwa uratibu na maandalizi kabambe ya mkutano huu ambao kwa wiki nzima hii mmesikika nchi nzima. Niwapongeze pia kwa moyo wenu wa kujitoa, nimeambiwa mlienda kutoa msaada katika shule ya Mzee wa Kimasai aliyejitolea kuanzisha shule kwa ajili ya watoto na wajukuu zake na sasa imekuwa pia ikihudumia majirani zake katika eneo la Mto wa Mbu hapa Arusha.

Sasa baada ya kusema hayo naomba nitamke rasmi kwamba **Kikao Kazi cha Maafisa Mawasiliano Serikalini kilichoanza tarehe 12/03/2018 kimefungwa rasmi leo 16/03/2018.**

Ahsanteni kwa kunisikiliza.